MWONGOZO WA NAMNA YA KUSHIRIKI KATIKA SOKO LA AWALI NA LA UPILI LA DHAMANA ZA SERIKALI ZA MUDA MREFU

MWONGOZO WA NAMNA YA KUSHIRIKI KATIKA SOKO LA AWALI NA LA UPILI LA DHAMANA ZA SERIKALI ZA MUDA MREFU

MNADA WA DHAMANA ZA SERIKALI

1.1 UTANGULIZI

Benki Kuu ya Tanzania kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, huuza Dhamana za Serikali za muda mrefu ikiwa ni njia ya kukopa fedha kutoka kwa ama taasisi au mwananchi mmoja mmoja.

Dhamana za Serikali za muda mrefu ni Dhamana zinazoiva muda zaidi ya mwaka mmoja. Dhamana za Serikali za muda mrefu kwa kiwango kikubwa huiwezesha Serikali kugharamia kwa muda nakisi katika bajeti yake inayosababishwa na upungufu wa mapato ukilinganisha na matumizi ya Serikali.

Dhamana hizi huuzwa kwenye soko la awali kwa njia ya ushindani kupitia minada na baada ya hapo uuzaji wa Dhamana hizo hufanywa kwenye soko la upili.

Ununuzi wa Dhamana za Serikali ikiwa ni njia mojawapo ya uwekezaji ina faida zifuatazo:

- Kuwekeza katika Dhamana za Serikali ni salama kwani Serikali haitarajiwi kukiuka mategemeo ya wadai wake wakati wa malipo.
- Dhamana za Serikali zinahamishika, hivyo mwekezaji anaweza kuziuza kabla ya muda wake wa kuiva endapo itakuwa ni lazima afanye hivyo.
- Dhamana za Serikali zinaweza kutolewa kama Dhamana kwa ajili ya mkopo.
- Dhamana za Serikali zina kiwango cha faida inayoridhisha.

Mwongozo huu umegawanyika katika sehemu kuu nne, nazo ni mfumo wa soko na namna ya kushiriki, mchakato wa mnada, utaratibu wa malipo na uuzaji wa Dhamana za muda mrefu katika soko la upili.

2.0 MFUMO WA SOKO NA NAMNA YA KUSHIRIKI

2.1 Mfumo Wa Soko

Kuna aina mbili ya Masoko ya Dhamana za Serikali za muda mrefu. Soko la awali ni pale ambapo Benki Kuu huuza Dhamana hizi kwa mara ya kwanza. Mnada hufanyika mara moja kwa mwezi. Uuzaji wa Dhamana hizo baada ya hapo hufanywa kwenye soko la upili.

2.2 Wanaostahili

Kila mkazi wa Tanzania anastahili kushiriki katika mnada wa Dhamana za Serikali za muda mrefu. Viwango vya kushiriki vimegawanyika katika sehemu mbili:

1. Wakala au mwekezaji mwenye kiwango cha kuanzia shillingi milioni tano (TZS 5,000,000.00) na kuendelea anaruhusiwa kushiriki moja kwa moja katika mnada wa Dhamana za Serikali.
2. Wawekezaji wenye kiwango cha pesa pungufu ya shilingi milioni tano wanapaswa kushiriki mnada kwa kupitia kwa mawakala.

2.3 Mfumo Wa Kuhifadhi Kumbukumbu

Benki Kuu ya Tanzania inao mfumo maalum wa kushughulikia na kuhifadhi taarifa zote za mnada wa Dhamana za Serikali za muda mrefu. Minada yote ya Dhamana hizo hufanyika na kumbukumbu zake huwekwa kwa njia za kielektroniki. Hivyo basi hakuna shahada au hati inayotolewa kwa wawekezaji.

3.0 MCHAKATO WA MNADA NA TARATIBU ZA KUTUMA ZABUNI

Benki Kuu ya Tanzania hutoa Dhamana za Serikali za muda mrefu na zinazoiva kwa nyakati tofauti. Dhamana hizi ni za muda wa miaka 2, 5, 7 na miaka 10.

3.1 Mpango na Utaratibu wa Utoaji wa Dhamana za muda mrefu

Benki Kuu ya Tanzania itatoa Tangazo la mpango na utaratibu wa utoaji wa Dhamana za Serikali za muda mrefu kila baada ya miezi mitatu. Mpango

huu utatolewa kupitia kwenye magazeti na utapatikana pia kwenye tovuti ya Benki Kuu ya Tanzania http://www.bot-tz.org Mpango huo utaonyesha kiwango kitakachotolewa na tarehe za minada.

3.2 Uitishaji wa zabuni

Tangazo kupitia vyombo vya habari (ambalo pia litakuwa **'prospectus'** tazama kiambatanisho na VI) litatolewa wiki moja kabla ya siku ya mnada.

3.3 Kuwasilisha Fomu Za Zabuni

Mawakala na wateja wao watapaswa kutumia fomu maalum za zabuni zinazoitwa **Fomu Za Benki Kuu Ya Tanzania-GB1** kwa ajili ya Dhamana za Serikali za muda mrefu (kiambatanisho I) wakati ambapo wawekezaji wanaoshiriki moja kwa moja watajaza fomu ziitwazo **Fomu Za Benki Kuu Ya Tanzania--GB2** (kiamabatanisho II). Fomu hizi zitapatikana Makao Makuu ya Benki Kuu ya Tanzania na katika matawi yake ya Arusha, Mwanza, Mbeya na Zanzibar. Aidha zinapatikana pia katika ofisi za mawakala waliosajiliwa.

Kiwango cha chini kabisa kuwekeza kwenye Dhamana za Serikali za muda mrefu ni shilingi milioni moja (TZS. 1,000,000) zikiwa katika mafungu ya shilingi laki moja (TZS.100,000)

Bei ya Dhamana za Serikali za muda mrefu zinapaswa kuwa na tarakimu nne za desimali. Aidha bei hizo zitaandikwa katika punguzo la mia ama zaidi ya mia na ama sawa na mia.

Wawekezaji watawasilisha fomu za zabuni kupitia kwa Mawakala au kupeleka moja kwa moja Benki Kuu ya Tanzania. Fomu hizo zilizojazwa zikiwa na saini ya mwombaji na muhuri zinatakiwa ziwasilishwe katika masanduku ya zabuni yaliyoko katika ukumbi wa mapokezi wa Makao Makuu ya Benki Kuu ya Tanzania, Mtaa wa Mirambo namba 10, Dar es Salaam au katika matawi ya Benki Kuu ya Tanzania yaliyoko Mwanza, Arusha, Mbeya na Zanzibar kabla ya saa tano kamili asubuhi siku itakayotajwa kuwa ya mnada wa Dhamana hizo.

Benki Kuu ya Tanzania inayo haki na uwezo wa kukubali au kukataa fomu mojawapo ya zabuni au zote zilizowasilishwa katika mnada husika.

3.4 Mgawanyo Wa Dhamana Zilizotolewa Kwa Wazabuni Walioshinda.

Benki Kuu ya Tanzania itaendesha mnada kwa kutumia mfumo wa kompyuta ujulikanao kama mfumo wa Dhamana za Serikali 'Government Securities Sytem' (GSS) ili kuwatambua washindi. Mfumo huu wa kompyuta hutumia mfumo wa bei tofauti. Kila mzabuni aliyeshinda atawajibika kulipia kwa bei aliyopendekeza.

Washindi wa zabuni wataorodheshwa, kwa kuanzia na bei ya juu zaidi hadi bei ya chini kabisa mpaka pale ambapo kiwango kilichotolewa kwa ajili ya mauzo ya Dhamana hizo yanamalizika.

Endapo washindi katika bei ya mwisho watahitaji kiwango cha Dhamana zaidi ya kiwango kilichobaki katika mafungu yaliyotolewa, Benki Kuu ya Tanzania itawagawia washindi wote kiasi kilichobaki kwa uwiano wa zabuni zao hadi kiwango kilichobaki kitakapomalizika.

3.5 Kutangaza Matokeo Na Kutoa Namba Ya Kutuma Malipo

Matokeo ya mnada yatatangazwa kwenye mbao za matangazo zilizopo Makao Makuu ya Benki Kuu ya Tanzania pamoja na matawi yake aidha pia matokeo hayo yatapatikana kwenye tovuti ya Benki Kuu ya Tanzania: http://www.bot-tz.org

Mawakala pia wataonyesha matokeo hayo kwenye ofisi zao.

Wazabuni watakaoshinda watapatiwa namba za malipo zitakazotolewa na Makao Makuu ya Benki Kuu ya Tanzania mara baada ya matokeo ya mnada kutolewa. Namba hizo za malipo zitatumika kama namba za marejeo kwa ajili ya kufanya malipo ya Dhamana za Serikali zilizonunuliwa kwa kupitia mfumo wa taifa wa malipo kati ya mabenki 'Tanzania Interbank Settlement System' (TISS).

4.0 MALIPO

4.1 Malipo Kwa Washindi Wa Mnada

- Wazabuni walioshinda watapaswa kulipia malipo ya Dhamana walizoshinda katika muda wa siku moja (T+1) baada ya mnada husika kufanyika.

- Benki za biashara na ambazo pia ni mawakala zitafanya malipo kupitia mfumo maalumu wa malipo kwa mabenki nchini (TISS).
- Wawekezaji wa moja kwa moja na mawakala wa soko la hisa la Dar es salaam watafanya malipo yao kwa kupitia benki za biashara, ambazo ni wanachama wa mfumo maalum wa malipo kwa mabenki nchini (TISS).
- Benki Kuu ya Tanzania itafanya malipo kwa niaba na kwa kupitia kwenye akaunti za benki za biashara ambazo si wanachama wa mfumo maalumu wa malipo kwa mabenki nchini na idara za kifedha ambazo si mabenki.
- Wazabuni walioshinda watapaswa kuwasilisha Benki Kuu ya Tanzania taarifa za akaunti zao za benki wanazotumia kwa ajili ya kuwezesha malipo ya Dhamana zao zitakapoiva.
- Endapo wazabuni walioshinda hawataweza kulipia zabuni zao ndani ya muda uliopangwa basi watazuiliwa kushiriki katika minada minne itakayofuata baada ya mnada walioshindwa kuulipia.

Taarifa inayoonyesha miliki ya Dhamana za Serikali alizonazo muwekezaji itatolewa kila inapohitajika.

4.2 Malipo Ya Mwisho Wa Kipindi Cha Uwekezaji:

Wawekezaji watalipwa faida mara mbili kwa mwaka. Faida hiyo itategemea kiwango cha riba kilichowekwa kwa kila Dhamana za Serikali za muda mrefu.

Muda wa kuiva kwa Dhamana za Serikali za muda mrefu utakapowadia, wawekezaji watalipwa thamani ya Dhamana pamoja na toleo la mwisho la faida.

Benki Kuu ya Tanzania itafanya malipo hayo kwa wawekezaji chini ya taratibu zifuatazo:

1. Kwa mabenki ya biashara ambayo ni washiriki wa mfumo wa malipo maalumu pamoja na wateja wao, Benki Kuu ya Tanzania itawalipa kupitia akaunti za mabenki hayo.
2. Kwa wale wawekezaji wa moja kwa moja, Benki Kuu itawalipa kupitia kwenye mabenki yao.

3. Kwa mabenki na idara za kifedha ambazo si mabenki na wala si wanachama wa mfumo maalumu wa malipo, Benki Kuu itafanya malipo moja kwa moja kwenye akaunti zao zilizoko Benki Kuu.

4.3 Kodi ya zuio

- Mapato yatokanayo na uwekezaji katika Dhamana za Serikali za miaka miwili yatalipiwa kodi ya zuio kwa mujibu wa taratibu za Serikali zitakazowekwa mara kwa mara.
- Aidha wawekezaji katika Dhamana za Serikali za miaka 5, 7 na 10 hawatalipia kodi ya zuio.
- Na aidha wawekezaji waliosamehewa kulipa kodi watapaswa kuwasilisha Benki Kuu cheti cha uthibitisho wa msamaha huo kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania.

5.0 UUZAJI WA DHAMANA ZA SERIKALI ZA MUDA MREFU KATIKA SOKO LA UPILI

- Dhamana za Serikali za muda mrefu zinasajiliwa katika soko la hisa la Dar es salaam (DSE).
- Dhamana za muda mrefu za Serikali zitauzwa katika soko la hisa la Dar es Salaam. Wawekezaji watakaopenda kununua au kuuza Dhamana za muda mrefu watakwenda kwenye soko la hisa kwa kupitia kwa madalali waliosajiliwa kuendesha shughuli za soko la hisa kwa ajili ya kupata taarifa zinazohusu taratibu za mauzo na manunuzi.
- Mara baada ya Dhamana hizi kuuzwa Soko la Hisa la Dar es Salaam litatuma taarifa zote za mauzo Benki Kuu ili kuiwezesha Benki kurekebisha taarifa zilizoko kwenye mfumo wake wa kumbukumbu za Dhamana za Serikali za muda mrefu.
- Uhamishaji wa Dhamana za Serikali baada ya soko la awali utafanywa kwa kuhamisha kumbukumbu katika vitabu vya kumbukumbu za wamiliki wa Dhamana za Serikali. Uhamishaji huo wa kumbukumbu, kutoka kwa mmiliki wa zamani na kwenda kwa mmiliki mpya utafanyika kwa kujaza fomu za uhamishaji wa Dhamana **FOMU ZA Benki Kuu**

YA TANZANIA-TF (kiambatanisho III). Fomu hizo zitajazwa nakala tatu.

- Muuzaji na Mnunuzi wa Dhamana za Serikali, kila mmoja wao atawasilisha Benki Kuu ya Tanzania fomu za uhamishaji wa Dhamana zilizojazwa sawia.
- Fomu za uhamishaji wa Dhamana za Serikali **FOMU ZA Benki Kuu YA TANZANIA-TF** zitapatikana Makao makuu ya Benki Kuu ya Tanzania, kwenye ofisi za matawi ya Benki Kuu ya Tanzania, aidha fomu hizo zinapatikana kwenye ofisi za mawakala waliosajiliwa.

MAWAKALA WALIOSAJILIWA:

Benki Kuu ya Tanzania imesajili mabenki na makampuni yafuatayo kufanya kazi za uwakala kwa wawekezaji katika Dhamana za Serikali:

- Akiba Commercial Bank Ltd.
- Citibank (T) Ltd.
- CRDB Bank Ltd.
- Diamond Trust Bank (T) Ltd.
- Eurafrican Bank (T) Ltd.
- Exim Bank (T) Ltd.
- Habib African Bank Ltd.
- International Bank of Malaysia (T) Ltd.
- Kenya Commercial Bank (T) Ltd.
- NBC Limited
- NMB Ltd.
- Stanbic Bank (T) Limited.
- Standard Chartered Bank Ltd.
- Orbit Securities Co. Ltd.
- Rasilimali Limited
- Solomon Securities Ltd.
- Core Securities Ltd.
- Tanzania Securities Ltd.
- Vertex International Securities.

Benki Kuu ya Tanzania inayo haki ya kufanya marekebisho kuhusu taratibu na mwongozo huu wakati wowote itakapokuwa ni lazima kufanya hivyo.

IDARA YA MASOKO YA NDANI

KURUGENZI YA MASOKO YA FEDHA

SEPTEMBER 2008

FARIHISI

Akaunti ya Dhamana: Akaunti inayotunzwa na Idara ya Masoko ya Ndani kwa ajili ya kuhifadhia kumbukumbu ya Dhamana zitolewazo kama dhamana kwa ajili ya mikopo.

Dhamana ya mkopo: Dhamana za Serikali ambazo hutolewa kwa ajili ya kudhamini mkopo na zinabakia kuwa hivyo kwa kipindi chote cha mkopo.

Akaunti ya hundi: Akaunti ambayo kila Dalali anapaswa kuwa nayo kwa ajili ya kuwezesha ufanyikaji wa malipo.

Akaunti ya umiliki: Hii ni akaunti inayohifadhi kumbukumbu za wawekezaji wote wa Dhamana za Serikali.

Akaunti ya pamoja: Hii ni akaunti inayosimamiwa na Idara ya Masoko ya Ndani ya Benki Kuu ya Tanzania ili kuwawezesha wawekezaji kupata taarifa sahihi kuhusu viwango vya Dhamana za Serikali wanazozimiliki katika muda husika.

Bei ya chini na ya mwisho katika kuuza Dhamana: Hii ni bei ya chini na ya mwisho inayokubalika katika kuuza na kuhakikisha kiwango cha Dhamana kilichotolewa kinamalizika.

Dhamana za Serikali: Huhusisha Dhamana za Serikali za muda mfupi na za muda mrefu zinazotolewa kwa mujibu wa sheria ya Mikopo na Dhamana ya mwaka 1974 kurekebishwa 2004.

Dalali: Mtu anayewaunganisha wanunuzi na wauzaji ili wafanye biashara. Mara nyingi huwatoza ushuru.

Kuiva kwa Dhamana: Hii ni tarehe ambayo Dhamana za Serikali zinalipwa baada ya kumalizika kwa kipindi cha uwekezaji kilichokubalika awali.

Mfumo wa malipo: Ni mfumo wa kubadilishana na kufanya malipo bila ya kutumia uhamishaji wa nyaraka au vyeti.

Mawakala: Haya ni mabenki ya biashara ambayo yamepewa leseni na Benki Kuu na taasisi ambazo zimesajiliwa na Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA). Wote hawa huwekeza katika Dhamana za Serikali kwa ajili yao binafsi au kwa niaba ya wateja wao.

Mfumo mkuu wa hifadhi: Hizi ni kumbukumbu zilizohifadhiwa kwa njia ama ya kawaida au kwa kutumia mfumo wa kompyuta. Mfumo huu ambao unasimamiwa na Benki Kuu ya Tanzania huhifadhi kumbukumbu zote zinazohusu umiliki wa Dhamana za Serikali

Mchuuzi: Mtu binafsi au taasisi ambayo hushiriki katika biashara ya Dhamana za Serikali kwa kununua na kuuza Dhamana hizo moja kwa moja.

Mauziano ya Dhamana za Serikali nje ya soko maalumu(OTC): Huu ni utaribu wa kuuza Dhamana kwa njia ya makubaliano kati ya muuzaji na mnunuzi bila kupitia kwenye masoko maalumu.

Namba ya malipo: Hii ni namba inayotumika na mabenki katika kutuma malipo ya Dhamana zilizonunuliwa kwenye mnada "bid code"

Soko la awali: Hili ni soko linalohusika na matoleo mapya ya Dhamana za Serikali kabla ya kumilikiwa na wawekezaji binafsi.

Soko: Uuzaji wa Dhamana za Serikali kati ya wanunuzi na wauzaji wa Dhamana za Serikali katika soko la wazi bila kuingiliwa na Benki Kuu ya Tanzania.

Siku ya malipo ya manunuzi: Ni siku ambayo Dhamana za Serikali hutolewa kwa washindi baada ya kulipia kiasi kinachotakiwa.

Siku Dhamana inapoiva: Ni siku ambayo Dhamana za Serikali zikiwepo zile za muda mfupi na za muda mrefu zinapoiva kwa malipo ya mwisho.

Taarifa ya akaunti: Hii ni taarifa inayotokana na akaunti ya pamoja inayowahusu wawekezaji ikionyesha hali halisi ya malipo yaliyofanyika na kiasi kilichopo katika akaunti za wawekezaji.

TISS: Huu ni mfumo wa malipo yanayofanywa moja kwa moja kwa njia za kielektroniki. Mfumo huu huwezesha malipo ya Dhamana za Serikali kufanyika kwa urahisi.

Thamani ya Dhamana: Thamani halisi ya Dhamana itakayolipwa pale Dhamana itakapoiva

Tarehe ya thamani: Ni tarehe ambayo uuzaji au ununuzi wa Dhamana unafanyika.

Utaratibu wa kurekodi kumbukumbu: Huu ni utaratibu wa kielektroniki wa kupitisha na kuhifadhi kumbukumbu pasipo kuhusisha ubadilishanaji wa hati au shahada zozote.

Wawekezaji wa moja kwa moja: Hawa ni wawekezaji wasiokuwa Madalali ambao huwekeza kiasi kisichopungua shilingi milioni tano kwa wakati mmoja.

Wachuuzi wa Mwanzo: Ni makundi ya washiriki ambao Benki Kuu ya Tanzania imewapa mamlaka ya kushiriki moja kwa moja kwenye soko la awali la Dhamana za Serikali na kisha kuziuza Dhamana hizo kwa umma.

MAULIZO YOTE YAWASILISHWE KWA:

Naibu Mkurugenzi
Idara ya Masoko ya Ndani
Benki Kuu ya Tanzania,
S.L.P 2939
Dar-es-Salaam
Tel: G/L 022 - 2110945-7
D/Line: 022 – 2233473-4
Fax: 022-2234049

Mkurugenzi wa Tawi,
Benki Kuu ya Tanzania,
S.L.P. 3043
Arusha,
Simu: 027 - 2508341-3/7091
Nukushi: 027 - 2508225/2508344

Mkurugenzi wa Tawi,
Benki Kuu ya Tanzania,
S.L.P 1362
Mwanza,
Simu: 028 - 2500313/2500315-8
Nukushi: 028 - 250074

Mkurugenzi wa Tawi,
Benki Kuu ya Tanzania
P.O Box 1203
Mbeya
Simu: 025 - 2503321-5
Nukushi: 025 - 2502844

Mkurugenzi wa Tawi,
Benki Kuu ya Tanzania S.L.P 568
Zanzibar
Simu: 024 - 2232140
Nukushi: 024 – 2231441

KIAMBATANISHO I

Fomu ya Benki Kuu ya Tanzania -GB1

Jina (Kwa herufi kubwa).....
Anwani :.....

Benki ya biashara

Tawi .....
Akaunti .....
Simu .....
Tarehe .....

Gavana,
Benki Kuu ya Tanzania
S.L.P. 2939,
Dar es Salaam.

YAH: MAOMBI YA KUNUNUA DHAMANA ZA Serikali ZA MUDA MREFU

Mimi /Sisi tunawasilisha zabuni ya kununua Dhamana za Serikali za Muda mrefu kama ifuatavyo:

Namba ya Toleo .....
Tarehe ya Mnada .....
Thamani shilingi.....
Thamani Kwa maneno.....
Bei .....
Endapo zabuni hii inaletwa kwa niaba ya mteja tafadhali andika jina kamili na anwani ya mteja huyo :
Jina.....
Anuani .....
Endapo zabuni tulizotuma zitashinda, tunatoa idhini kwako kuchukua kiasi cha fedha linganifu kwa ajili ya kulipia Dhamana za Serikali kutoka kwenye akaunti yetu ya hundi.

Tarehe	Saini Iliyoruhusiwa	Saini iliyoruhusiwa

Fomu zote sharti zipigwe muhuri rasmi.

KIAMBATANISHO II

Fomu za Benki Kuu ya Tazanaia -GB2

Jina (Kwa herufi kubwa) .....
Anwani :.....
Benki ya biashara.....
Tawi.....
Akaunti .....
Simu .....
Tarehe .....

Gavana.
Benki Kuu ya Tanzania
S.L.P. 2939,
Dar es Salaam.

YAH: MAOMBI YA KUNUNUA DHAMANA ZA Serikali ZA MUDA MREFU

Mimi /Sisi tunawasilisha zabuni yetu ya kununua Dhamana za Serikali za Muda mrefu kama ifuatavyo:

Namba ya Toleo .....
Tarehe ya Mnada .....
Thamani shilingi .....
Thamani Kwa maneno .....
Bei .....

Mimi/Sisi tuko tayari kulipa kwa ajili ya kiwango hicho tulichoomba au kiwango chochote tutakachopewa.

Mimi /sisi tunaahidi kufuata na kuzingatia sheria na taratibu zinazotawala utoaji na uuzaji wa Dhamana za Serikali

Wasaalam .....

KIAMBATANISHO III

Fomu za Benki Kuu ya Tanzania -TF

FOMU ZA UHAMISHO:

Fomu Ya Uhamisho Wa Dhamana Za Serikali.

1.0 Jina la Muuzaji* .....

2.0 Jina la Mnunuzi* .....

2.1 Namba ya mficho ya Muuzaji .....

2.2 Namba ya mficho ya Mnunuzi .....

3.0 Ni kwa niaba ya mteja wa muuzaji? Ndiyo/Hapana

3.1 Kama jibu ni ndiyo, taarifa za mteja zitajwe:

Jina .....

3.2 Kama jibu ni hapana, basi itakuwa kwenye akaunti binafsi ya Mnunuzi

4.0 Ni kwa niaba ya mteja wa mnunuaji? Ndiyo/Hapana

4.1 Kama jibu ni ndiyo, taarifa za mteja zitajwe:

Jina .....

4.2 Kama jibu ni hapana , basi itakuwa kwenye akaunti binafsi ya Mnunuzi

5.0 Kumbukumbu ya Dhamana namba: .....

6.0 Tarehe ya thamani: .....

7.0 Thamani halisi ya Dhamana .....

8.0 Bei kwa kila shilingi mia moja .....

9.0 Kiwango kilichopunguzwa .....

10.0 Aina ya uhamisho .....

10.1 Ununuzi na uuzaji wa moja kwa moja /

10.2 Dhamana

Endapo unanunua au unauza futa 10.2

Na endapo unaweka kama dhamana ya mkopo futa 10.1

11.0 Muuzaji

Mimi / Sisi ambao ni wauzaji tunatoa idhini kwa Benki Kuu ya Tanzania kuhamisha kiwango cha fedha/Dhamana tajwa kutoka kwenye akaunti yangu/ya mteja wangu na kuziweka kwenye akaunti ya Mnunuzi/ Mteja wa Mnunuzi .

12.0 Mnunuzi

Mimi / Sisi ambao ni wanunuzi tunatoa idhini kwa Benki Kuu ya Tanzania kuhamisha kiwango cha fedha/Dhamana zilizopunguzwa kutoka kwenye akaunti yangu/yetu na kuziweka kwenye akaunti ya hundi ya Muuzaji.

Tarehe	Saini iliyoruhusiwa	Saini iliyoruhusiwa

Kwa Matumizi ya Ofisi tu	**Kumbukumbu ya malipo namba**
A. Idara ya masoko ya ndani Tarehe/Muda wa kupokelewa ... Imekaguliwa na ..... **B. Idara ya malipo ya ndani** Tarehe/ muda wa kupokelewa na ..... Imekaguliwa na..... Malipo yamefanyika na	Imepokelewa na ..... Imeidhinishwa na..... Imepokelewa na..... Imeidhinishwa na ..... Uhamisho wa Dhamana umefanyika na .....

* Alama hii inaonyesha Muuzaji na Mnunuzi katika soko baada ya toleo la awali.

Fomu lazima zipigwe muhuri wa ofisi.

Uhamisho wa milki ya Dhamana utafanyika pale tu fomu za kuuzia na fomu za kununulia zitakapopokelewa na Benki Kuu ya Tanzania.

KIAMBATANISHO IV

MFANO WA TANGAZO

BENKI KUU YA TANZANIA

DHAMANA ZA SERIKALI ZA MIAKA MIWILI ZENYE FAIDA YA ASILIMIA 7.82%

TOLEO NAMBA 255 MNADA NAMBA 3 UTAKAOFANYIKA TAREHE 21-6-2006

Benki Kuu ya Tanzania kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inakaribisha wazabuni kwa ajili ya ununuzi wa Dhamana za Serikali za miaka miwili iliyotajwa hapo juu. Kanuni na Masharti ya Dhamana hii ni kama ilivyoanishwa hapa chini;

1.	**Mtoaji**	Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
2.	**Kiwango kinachotolewa**	Shilingi za Tanzania, Bilioni nne (4)
3.	**Taratibu za zabuni**	Fomu za zabuni ziwasilishswe katika sehemu ya mapokezi ya makao makuu ya Benki Kuu mtaa wa Mirambo namba 10, Dar es salaam au kwenye ofisi za matawi ya Benki Kuu zilizoko Mwanza, Arusha, Mbeya na Zanzibar na kutumbukizwa kwenye masanduku ya zabuni kabla ya saa tano kamili asubuhi ya siku ya mnada
4.	**Tarehe ya mnada**	Jumatano, tarehe 21 -6-2006
5.	**Tarehe ya kufanya malipo**	Alhamisi, tarehe 22- 6- 2006
6.	**Hifadhi ya kumbukumbu**	Kumbukumbu zote za Dhamana zitahifadhiwa kwa kutumia mfumo wa kompyuta.

MFANO

7.	**Bei kwa kila shilingi mia (100)**	Bei zindikwe zikiwa na tarakimu mbili za desimali. Aidha bei hizo zitaandikwa katika punguzo la mia ama zaidi ya mia na ama sawa na mia.
8.	**Matokeo ya Mnada**	Matokeo ya mnada yatatangazwa kwenye mbao za matangazo zilizopo Makao Makuu ya Benki Kuu katika ofisi za matawi yake zilizopo Arusha, Mbeya, Mwanza, na Zanzibar na pia katika tovuti ya Benki Kuu ya tanzania Http://www.bot-tz..org.
9.	**Kiwango cha chini cha zabuni kinachoruhusiwa**	Kiwango cha chini kwa kila zabuni lazima kiwe shilingi 1,000,000/= kwa wawekezaji watakaopitia kwa madalali na kiwango cha chini lazima kiwe shilingi 5,000,000/= kwa wawekezaji wa moja kwa moja. Ongezeko la zabuni kutoka kiwango cha chini lazima liwe kwa kiasi kinachoweza Kugawanyika Kwa makumi ya shilingi 100,000/= bila kubaki.
10.	**Tarehe za kulipa faida (riba)**	Ni kila Tarehe 26 Mwezi wa kumi na tarehe 27 Mwezi wa nne. Siku za malipo haya huanza kuhesabiwa mara baada ya kulipia Dhamana hii.
11.	**Namna ya kuhesabu siku**	Siku halisi /365
12.	**Riba ya Dhamana**	Ni 7.82% p.a

MFANO

13. **Kodi**	Faida itakayopatikana itatozwa kodi ya zuio kwa kiasi cha asilimia kumi (10%)
14. **Sarafu**	Mnada utaendeshwa kwa shilingi za Tanzania tu.
15. **Tarehe ya kuiva**	27-04-2008
16. **Kusajili Dhamana kwenye Soko la Hisa la Dar es salaam**	Dhamana hii itasajiliwa na kuwa tayari kwa kuuzwa kwenye soko la upili tarehe 27-6-2006
17. **Wazabuni watakaoshindwa kulipia**	Wazabuni watakaoshinda na kushindwa kulipa zabuni zao walizoshinda ndani ya muda uliopangwa watanyimwa haki ya kushiriki katika minada minne inayofuatia mfululizo.
18. **Maelezo mengine**	Itokeapo kwamba kiwango kilichotolewa hakikununuliwa chote, Benki Kuu itakinunua kiwango hicho kilichobakia kwa bei ya wastani wa bei zilizoshinda kwenye mnada huo "WAP"

Benki Kuu ya Tanzania inayo haki ya kukubali au kukataa zabuni yoyote.

Kwa maelezo zaidi wasiliana na Idara ya Masoko ya Ndani,
Benki Kuu ya Tanzania,
Mtaa wa Mirambo Namba 10,
S.L.P. 2939 Dar es Salaam.
Namba za simu 2233481-90, 2233473-4, nukushi 2234049
na tovuti: www.bot-tz.org

MFANO

Benki Kuu ya Tanzania
S. L. P 2939, Dar-es-Salaam